**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU- TAMISEMI

Namba ya usajili (NECTA) : S6363
Mkuu wa Shule: 0753188737
Makamu Mkuu wa Shule:
0759876910
Mwl. Malezi: 0761495611
Patron: 0612026998
Shule ya Sekondari NDOLEZI
S.L.P.76, MAFINGA
Tarehe.................................

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi...........

______________________________

S.L.P............................................

______________________________

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NDOLEZI, HALMASHAURI YA MJI IRINGA, MKOA IRINGA**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shute hii na atasoma tahasusi ya...........

Shule ya Sekondari NDOLEZI ipo umbaliua Kilometa 10 utoka stendi kuu ya mabasi ya Mji wa Mafinga. Usafiri wa kufika shuleni unapatikana katika kituo cha mabasi Mafinga Mjini. Nauli ni Shilingi 5000/= kwa pikipiki na Shilingi 3000/= kwa bajaji na Shilingi 5000/= kwa taksi. Muhula wa Masomo unaanza tarehe ………………….. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ……………. Na mwisho wa kuripoti ni tarehe ………………

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia:**

**SARE ZA SHULE - WAVULANA**

- Suruali mbili (02) kitambaa ZABIBU zilizoshonwa kwa heshima iwe na mkunjo chini (turnerup). Marufuku mishono ya JEANS AU MLEGEZO, AU suruali inayobana (kitambaa kimeambatanishwa) Upana wa chini uwe 17cm.
- Mashati mawili meupe ya mikono mirefu yasiyoangaza.
- Koti Rangi ya ZABIBU lililoshonwa kwa Heshima ili kufanya suti lisiwe na mipasuo nyuma. (Tunashauri ushonewe sare za Shule kwa mafundi wa hapa Mafinga kuepuka kuchanganya rangi / Kitambaa).
- Tai iliyoshonwa kwa Heshima ya kitambaa ZABIBU bila maua.
- Viatu vya ngozi jozi mbili (02) rangi nyeusi vya kamba, Boots na viatu vya kuchomekea haviruhusiwi kabisa.
- Soksi jozi za kumtosheleza muhula au nusu muhula rangi nyeusi.
- Mkanda wa suruali — rangi nyeusi (usio na urembo)
- Nguo za kushindia (shamba dress) suruali mbili (2) za light blue mshono sawa na sare ya Shule zitapatiana shuleni kwa gharama ya tsh.32,000/= kwa anayehitaji.
- Pulneck nyeupe na Jacketi zito jeusi.
- Truck suit rangi ya kijivu Nzito zenye mistari miwili pembeni pea moja (zinapatikana shuleni kwa shilingi 25,000/= kwa anayehitaji)
- Jezi ya michezo rangi blue bahari ya Manchester city (bukta na t-shirt) na viatu aina ya Njumu.
- Raba nyeupe.
- Viatu vya michezo kulingana na mchezo anaocheza.
- T-shirt mbili (02) zinapatikana shuleni @15,000/= JUMLA 30,000/=

NB: Nguo nyingine haziruhusiwi.

2.1 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi wote wanapaswa kuja nayo shuleni:-

i Ream ya karatasi 02 (A4 photocopy paper) Kwa mwaka.
ii Godoro la futi 2 % kwa futi 6 livalishwe cover kama la hospitali.
iii Mashuka pea 2 rangi ya pink na ligt bluu, blanketi 1 nzito, mto 1 Na foronya 2 rangi ya pinki na chandarua kimoja (01
iv Vyombo vya chakula containa, kijiko, jagi la kuogea na kikombe.
v Ndoo 2 zenye mfuniko, ujazo wa lita kumi (10)
vi Kandambili jozi Kila mzazi/mlezi unaombwa kumpa fedha ya matumizi yake binafsi ikiwemo nauli ya kwenda na kurudi nyumbani wakati wa likizo
vii Aje na Nakala (coppy) ya cheti cha kuzaliwa.
viii Viatu vya wazi (Sandles) za kufunga au simple shoes HAVIRUHUSIWI.
ix Tranka la chuma 01. Mafuta ya kupaka, dawa ya meno, mswaki, sabuni n.k (MANUKATO KAMA PAFYUMU NA CREAM HAZIRUHUSIWI).

x Taulo
xi Dissecting kit 01
xii Scientific calculator 01
xiii Stop watch 01.
xiv Sabuni ya Maji lita tano (5).
xv Tochi au taa ya Solar kwa dharula Umeme ukikatika.
xvi Nguo za ndani za kutosha
xviiKwanja 01, jembe 01, squizer 01, raki 01, na mifagio 02 (Soft brum na hard brum)

NB. TUNASHAURI MZAZI/MLEZI AMKATIE BIMA YA AFYA MWANAFUNZI
Kwa wale ambao hawana bima ya afya tunashauri aje na kiasi cha 50,400/= kwa ajili ya bima ya afya kwa mwaka.

MAHITAJI YA TAALUMA

i) Daftari counter book Q3 ziwe 15 na daftari ndogo 15.
ii) Peni, pencil, ruler na mkebe. nk.
iii) Vitabu vya masomo ya Tahasusi husika atakayosoma kama vile PCB, PCM na PGM iv) Faili 02 (Sping files).

ANGALIZO: Mwanafunzi alete kifaa kulingana na tahasusi anayosoma.

2.1 Michango mbalimbali

Shule za Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha hii ilipwe kwenye akaunti ya shule 60210076982 NMB Bank kwa Jina la NDOLEZI SEKONDARI na wasilisha pay in slip kwa Mhasibu wa Shule ikiwa imeandikwa jina la Mwanafunzi.

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na OWM - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);

iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari.
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na** hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;
- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;
- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

**3.2 Makosa yatakayo sababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

a) Wizi;
b) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
c) Kugoma na kuhamasisha mgomo;
d) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
e) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
f) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
g) Kufuga ndevu;
h) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
i) Uvutaji wa sigara;
j) Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
k) Kupata ujauzito au kutoa mimba;
l) Kusababisha mimba;
m) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
n) Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
o) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
p) Kudharau Bendera ya Taifa;
q) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
r) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**3.3 Viambatisho na Fomu Muhimu**

i Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

4.Tafadhali soma kwa makini maelezo kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

HONGERA

NB: Kwa siku za hivi karibuni kum na BK (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe m upi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

> Mkuu wa shule: 0753188737
> Makamu Mkuu wa Shule: 0759876910
>MwandamiziTaaluma :0764981368
>MwandamiziMalezi: 0712906525

I. FOMU YA MAELEZO BINAFSI KUHUSU HISTORIA YA MWANFUNZI IMKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

____________________

____________________

____________________

MKUU WA SHULE, SHULE YA SEKONDARI NDOLEZI,
S.L.P. 76.
MAFINGA

**YAH: KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NDOLEZI ILIYOKO MAFINGA- MKOA WA IRINGA**

Mimi mwanafunzi.__________________________ Kidato cha..........
Mwaka...........

1. Nilizaliwa mnamo mwaka (Taja tarehe, mwezi na mwaka)...........
kijiji/Mjini...........

Nimesoma Shule ya sekondari ya......................................Wilaya ya ................ Mkoa wa ....................

- Nilikuwa kiongozi wa………………………………………
- Sikuwa kiongozi ……………………………………………
- Michezo niipendayo ni...................................................................
- Nina kipaji cha.....................................,..................
- Mengineyo Niwezayo.........................................................

2. Naahidi kuwa mtiifu wa sheria za shule, kutoshiriki katika mgomo, fujo, makosa ya jinai, dharau kwa walimu, dharau kwa viongozi wa ngazi zote au wowote wale. Nitakuwa na nidhamu ya kujituma, kusoma kwa bidii na kuwa mfano bora kwa wanafunzi wengine.Tofauti na haya niondolewe shuleni mara moja.

Jina la_mwanafunzi …………………………. sahihi …………………. Kidato ………….tarehe ……………….

2. FOMU YA MZAZI/MLEZI KUKRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE HALAL! YATAKAYOTOLEWA NA SHULE

__________________________

__________________________

__________________________

MKUU WA SHULE,

SHULE YA SEKONDARI NDOLEZI,

S.L.P. 76,

MAFINGA

**YAH: KUKUBALI KUJIUNGA MWANANGU NA SHULE YA SEKONDARI NDOLEZI ILIYOKO MAFINGA-MKOA WA IRINGA**

MWANAFUNZI …………………………………..

KIDATO CHA TANO MWAKA 2026

1. Mimi……………………………………………………………
   Mzazi /mlezi wa mwanafunzi aliyetajwa hapo juu. Nakiri kuwa nimeelewa maelekezo yote yaliyotolewa na masharti ya fomu hii.
2. Nakubali mwanangu aendelee na masomo na nitatekeleza yale yote yanayonihusu kwa wakati wake. Kama ilivyoagizwa katika maelekezo ya kujiunga na shule.
3. Naahidi kumhudumia mtoto wangu kwa hali na mali ili kufikia malengo yake ya kujiunga na Shule hii.
4. Naahidi kusimamia nidhamu na maendeleo yake muda wote awapo hapa shuleni.
5. JINA LA MZAZI/MLEZI ……………………………………. SAHIHI…………………
6. ANWANI YA MZAZI/MLEZI…………………….
7. NAMBA YA SIMU ……………………TAREHE …………………………..

FOMU YA KUPIMA AFYA YA MWANAFUNZI

03. (FOMU YA KUPIMA AFYA YA MWANAFUNZI)
SEHEMU A

SHULE YA SEKONDARI NDOLEZI,

S.L.P. 76,

MAFINGA

KUMB.NA.MTC/NDLSS/J1/2026/F5/01

MGANGA MKUU,

HOSPITALI YA SERIKALI YA

________________________________

S.L.P ………………..
MAFINGA

YAH: FOMU YA KUPIMWA AFYA YA MWANAFUNZI

Somo la hapo juu lahusika.

Tafadhari tunaomba umpime mwanafunzi aliyetajwa hapo juu wa kidato cha TANO mwaka 2026; kwa gharama za mzazi/mlezi wake.

Ni muhimu apimwe ili kujua afya yake kabla ya kuripoti hapa shuleni na kuendelea na masomo.

Natanguliza shukrani

………………………………………

HONGERA S.SWENYA

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE ★ S.L.P 76 MAFINGA ★ NDOLEZI SEKONDARI

3. FOMU Hli IJAZWE NA MGANGA WILAYA NA MWANAFUNZI AJE NAYO SHULENI NA KUIKABIDHI KWA MKUU WA SHULE.

SEHEMU B

Mimi (Jina la Mganga Mkuu wa Mkoa/Wilaya) ……………………………………

Ninathibitisha kuwa mwanafunzi huyu (Jina la mwanafunzi) ……………………………..

Amepimwa na mimi kikamilifu na kuonekana kuwa anayo /hana afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo;

(A) Hali ya Mwili.

i Mapigo ya moyo ……………………………………..
ii Damu (Haemoglobin) ………………………………..
iii Kundi la Damu (Blood group …………………………………………
iv Mkojo …………………………
v Haja kubwa ………………………………..
vi Macho ……………………………………..
vii Masikio …………………………………….

NB. Weka maoni yako kuhusu kile kilichotajwa. ……………………………………………...
………………………………………………………………………………………………

(B) Magonjwa.

Amewahi/hajawahi au hana magonjwa yafuatayo;

(a) Kifua kikuu (TB) ………………………………
(b) Kifafa (Epilepsy) ……………………………..
(c) Shinikizo la damu (BP) ……………………..
(d) Magonjwa ya tumbo ………………………..
(e) Selimundu (Sickle cells) ……………………
(f) Ukoma ………………………..
(g) Magonjea ya zinaa (taja aina) ……………….
(h) Ugonjwa wa akili …………………………
(i) Ugonjwa mwingine nje ya orodha hapo juu ………………….

Maoni ya daktari ……………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………….

Saini na Muhuri wa Daktari/Mganga wa Hospitali ya Serikali